# KISWAHILI : WIKI YA KWANZA
## JUMATATU

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata**

Nchi nyingi duniani zimejengwa na watu wa makabila tofauti. Tofauti hizi za makabila ni sehemu ya utajiri wa utamaduni wa taifa. Hata hivyo, wakati mwingine watu husahau umuhimu wa umoja na kuanza kujitenga kwa misingi ya ukabila. Ukabila ni hali ambapo mtu hupendelea watu wa kabila lake na kuwadharau watu wa makabila mengine.

Ukabila unaweza kuleta madhara makubwa katika jamii. Kwanza husababisha chuki na migogoro kati ya watu. Badala ya kuishi kwa amani, watu huanzakugombana na kutengana. Pili, ukabila huathiri maendeleo ya taifa kwa sababu watu huchagua viongozi kwa misingi ya kabila badala ya uwezo. Hali hii husababisha ukosefu wa haki na kudhoofisha maendeleo ya jamii.

Aidha, ukabila huweza kuharibu urafiki na mshikamano kati ya wananchi. Watu wanaanza kuogopana na kutoaminiana. Jamii inayokosa umoja huwa dhaifu na haiwezi kupiga hatua mbele.

Ili kuondoa tatizo hili, jamii inapaswa kuhimiza umoja, upendo na heshima kwa watu wote bila kujali kabila lao. Shuleni, wanafunzi wanaweza kujifunza kuishi pamoja na kuheshimiana. Viongozi pia wanapaswa kuhubiri amani na usawa kwa wananchi wote. Tukikataa ukabila na kuthamini tofauti zetu, tutajenga taifa lenye amani, maendeleo na mshikamano.

1. Eleza maana ya tamaduni kulingana na kifungu hiki

___

2. Bainisha athari zozote mbili zinazotokana na ukabila kulingana na kifungu hiki

___

3. Ni vipi jamii inaweza kupambana na tatizo la ukabila ili kuafikia utangamano na mshikamano katika jamii

___

4. Fafanua dhana ya ukabila kulingana na kifungu hiki

___

5. Andika faida moja inayopatikana kwa kuishi kwa amani bila kuongozwa na ukabila

___

6. **"Tukikataa ukabila na kuthamini tofauti zetu"**, ni nini maana ya kauli hii.

___

Parent's/Guardian's Signature ____________________ Date ____________